**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Ishirini na Tano – Tarehe 05 Juni, 2021.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa mwaka 2021/2022.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi:**

Hotuba ya Kamati ya Uchumi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa Mwaka 2021/2022.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

218. MHESHIMIWA PROF.OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Serikali kupitia Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana imekuwa ikipokea misaada mbali mbali ndani na nje ya nchi, lengo likiwa ni kupunguza umasikini na utegemezi haswa kwa mafukara, licha ya uwepo kwa Kamisheni hiyo bado kumekuwa na wimbi kubwa la ongezeko la umasikini.

(a) Je, Serikali imejipanga vipi kwenye kutoa elimu ya Wakfu ili wananchi wengi wapate uelewa zaidi wa jambo hilo na kuweza kuchangia.

(b) Je, Serikali ina mipango gani ya kuziimarisha taasisi za kutoa misaada (Charitable societies) zisizo za kidini kuchangia zaidi na kuinua pato la Taifa.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

135. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Usimamizi wa elimu katika Mabaraza ya Manispaa na Halmashauri unatafautiana katika muundo wa uongozi kati ya Baraza au Halmashauri moja na nyengine.

(a) Je, kwa nini Serikali haitowi muongozo utakaoweka muundo wa aina moja kwa Mabaraza na Halmashauri zote.

(b) Kwa nini katika ngazi za msingi hakuna Afisa Elimu anaesimamia Mkoa kama ilivyo kwa ngazi ya Sekondari.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

62. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Sheria za Zanzibar na Tanzania Bara zinaeleza wazi kuwa mgeni yeyote hawezi kuruhusiwa kufanya kazi nchini hadi awe na vibali vya kazi na vya ukaazi. Hata hivyo, wapo baadhi ya wageni ambao wanafanyakazi hapa Zanzibar bila ya kuwa na vibali vya kazi, jambo ambalo ni kinyume na Sheria.

(a) Kwa nini Serikali inashindwa kuwachukulia hatua za kisheria watu hao ambao wanavunja Sheria za nchi.

(b) Zipo tetesi kwamba watu hao wasio na vibali wanajihusisha na biashara haramu za dawa za kulevya, Je, Serikali inasemaje juu ya tuhuma hizo.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

82. Mheshimiwa Kombo Mwinyi Shehe (Jimbo la Wingwi) - Ataamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Wenye maduka ya kuuza kanda za wasanii mbali mbali wamekuwa wakikumbana na mrundikano wa kodi za kulipia taasisi mbali mbali kama vile Baraza la Sensa na Filamu (BASFU), Hakimiliki (COSOZA), pamoja na Serikali za Miji na Wilaya, huku wauza kanda wenyewe wakiuza kanda moja kwa bei ya Tshs 500 pekee.

(a) Je, Serikali haioni kuwa kufanya hivyo hakuwasaidii wasanii wetu bali wanazidi kuwadumaza.

(b) Je, ni lini kodi hizo zitaondolewa na angalau kubakishwa kodi moja tu.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

28. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani)

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Daraja liliopo kijiji cha Vitongoji ni kiungo muhimu baina ya Kware ya mawe na kifusi iliyopo Makaani pamoja na miji yote ya Pemba. Kwa sasa daraja hilo limeanza kuchakaa na ukiangalia kwa ndani tayari nondo zake zimeanza kufanya kutu na kukatika vipande vipande. Kwa kuwa daraja hilo hupitwa na magari ya abiria pamoja na magari yenye uzito mkubwa yaliyobeba kifusi, mawe na mchanga.

(a) Je, ni lini Serikali itakwenda kuangalia hali ya daraja hilo.

(b) Je, ni lini Serikali italifanyia ukarabati daraja hilo.

146. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Serikali imetumia fedha nyingi kununua mtambo wa lami uliopo Kibele ambao unahitaji matunzo ili uweze kutumika kama ilivyokusudiwa.

Je, ni lini Serikali itachukuwa hatua ya kuujengea banda la kuuhifadhi mtambo huo.

**<u>Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:</u>**

185. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani)-

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Katika malengo ya mwaka 2020/2021 Serikali ilikusudia kukamilisha ujenzi wa hospitali maalum ya kutibu wagonjwa wenye maradhi ya kuambukiza (Highly Infectious Treatment Centre) katika eneo la Dunga.

(a) Je, lengo hili unalifahamu.

(b) Je, ujenzi huo umefikiwa wapi mpaka sasa.

**III. <u>HOJA ZA SERIKALI:</u>**

**<u>Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa Mwaka 2021/2022.

**Zanzibar,**
**05 Juni, 2021.**

**(Raya Issa Msellem)**
**<u>KATIBU WA BARAZA</u>**